**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MWONGOZO WA BIASHARA KWA KUTUMIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA ULIYOTOLEWA CHINI YA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA (TCDC), BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA (WRRB) NA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX) WA MWAKA 2021 KWA MAZAO YA: -

-

1. **CHOROKO**
2. **SOYA**
3. **UFUTA**
4. **MBAAZI**
5. **DENGU**

**JANUARI, 2021**

## UTANGULIZI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania kwa pamoja wana jukumu la kuhakikisha kuwa hali ya kipato cha mkulima inaimarika kupitia uzalishaji wa mazao yenye ubora na yaliyoongezwa thamani ili kukidhi mahitaji ya soko. Vilevile, kuweka mifumo imara ya masoko ili kumpatia mkulima soko la uhakika na bei yenye tija kwa mazao yake.

Ili kuwa na upatikanaji wa soko la uhakika na uimara wa bei, Taasisi hizi zimekusudia kuwepo kwa Mfumo imara wa uzalishaji, ukusanyaji, utunzaji, uuzaji na malipo ya mazao yanayozalishwa.

Kwa kutambua umuhimu wa mfumo wa mauzo katika kuimarisha masoko ya bidhaa za wakulima na kupunguza changamoto zitokanazo na bei, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa la Tanzania wameandaa mwongozo wa biashara ya mazao ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu utakaotekelezwa katika mikoa inayolima mazao hayo ili kuhamasisha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kumtafutia soko mkulima kupitia Vyama vya Ushirika.

Mwongozo huu utatambulika kama "**Mwongozo wa biashara kwa kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala uliyotolewa chini ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa tanzania (TMX) wa mwaka 2021 kwa mazao ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu**".
Mwongozo huu unahusu utaratibu wa Biashara ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu inayozalishwa hapa nchini.

**SEHEMU YA KWANZA**

**TAFSIRI YA MAANA YA MANENO YALIYOTUMIKA**

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

***''Sheria''*** maana yake ni sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya Mwaka 2013, Sheria ya Stakabadhi za Ghala sura 339RE 2016 pamoja na Sheria ya Soko la Bidhaa ya mwaka 2015.

***''Ghala la chama cha msingi''*** maana yake ni kituo cha kukusanyia Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu za wakulima kwa ajili ya kuzipeleka katika ghala kuu la mnada.

*"***Ghala la mnada*****"** maana yake ni ghala lililokidhi sifa na vigezo kwa ajili ya kukusanya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu za wakulima yatakayouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

***''Kamati ya mauzo''*** maana yake ni kamati inayoundwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Sekreterieti za Mikoa kwa lengo la kuendesha na kusimamia minada ya mazao ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu katika Mikoa husika.

***''Lot''*** maana yake ni fungu la mazao yaliyopo katika ghala la mnada zinazosubiri kuuzwa kwenye mnada.

***''Katalogi ya mauzo''*** maana yake ni kijarida cha mauzo ya mazao (sales catalogue) kinachoonesha aina ya zao, idadi katika kilo, ubora, loti na ghala la mnada mazao husika yalipohifadhiwa.

***"Mfumo wa Stakabadhi za Ghala" maana*** yake ni mfumo wa soko ambapo mazao huhifadhiwa katika Ghala Kuu lililopatiwa Leseni na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kutolewa stakabadhi ikionesha kiasi, ubora na daraja la mazao kwa lengo la kusubiri kuuzwa.

***''Mhakiki wa Ubora''*** maana yake ni mtaalam aliyefuzu mafunzo ya uhakiki

ubora wa mazao na kupata cheti kutoka mamlaka ya zao husika na kuajiriwa na Mwendesha Ghala kwa ajili ya kuhakiki ubora wa mazao yanayoingia katika Ghala Kuu.

***‘‘Mkaguzi wa Ubora’’*** maana yake ni mtaalam wa kukagua ubora wa mazao yaliyopo kwenye ghala, gari, shamba, kiwanda na mahali pengine popote ambapo panapohusika na Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu.

***‘‘Mnunuzi’’*** maana yake ni mfanyabiashara aliye na leseni ya ununuzi wa mazao aliyesajiliwa na mamlaka husika.

***‘‘Msafirishaji’’*** maana yake ni kampuni inayohusika kusafirisha mazao kwa mujibu wa taratibu zilizopo

***“Mwendesha ghala/Mtunza ghala”*** Kampuni iliyosajiliwa na Bodi kujishughulisha na biashara ya kuendesha ghala kwa ajili ya, pamoja na mambo mengine, kupokea na kuhifadhi mazao jamii ya kunde kwa mujibu wa Sheria ya Sakabadhi za Ghala Sura ya 339(RE 2016)

***“Mazao bila Daraja (BD)”*** Ni mazao ambayo hayajapewa daraja lakini yamezingatia viwango vya usafi, unyevu, rangi na umbo**.**

***‘‘PDN’’ (Produce Dispatch Note)*** maana yake ni hati ya kusafirisha mazao ndani ya nchi.

***‘‘TBS’’ (Tanzania Bureau of Standards)*** maana yake ni Shirika la Viwango Tanzania.

***“Short Sale” Maana*** yake ni mauzo ya mazao ambayo hayajatangazwa kwenye Mwongozo wa mauzo (Sales Catalogue).

***‘‘Akaunti ya Pamoja’’*** maana yake ni akaunti iliyofunguliwa benki na Chama Kikuu cha Ushirika kwa ajili ya kudhibiti mtiririko wa fedha za malipo ya mazao kutoka kwa wanunuzi kwenda akaunti za vyama vya msingi ikiwa ni pamoja na wakulima na walipwaji wengine kwa kuzingatia mjengeko wa bei.

***‘‘Hati Shinikizi ya Malipo’’*** maana yake ni nyaraka itakayosainiwa na mnunuzi mbele ya chama kikuu husika inayoonesha wajibu wa mnunuzi kulipia mazao aliyoshinda kwenye mnada.

***''TRA''* (Tanzania Revenue Authority)** maana yake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania.

***''WMA''* (Weights and Measures Authority)** maana yake ni Wakala wa Vipimo Tanzania.

"**Chama cha Msingi"** maana yake ni Chama cha Msingi cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013.

**"Chama kikuu"** maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013.

**"Mweka mali"** Mkulima/mwakilishi au wakala wa mkulima wake aliyerasimishwa kuweka mali zake ghalani.

**SEHEMU YA PILI**
**MADHUMUNI YA KUTUMIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KATIKA MAZAO YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, MBAAZI NA SOYA**

2.1 **Lengo kuu la kutumia Mfumo**

Kuwezesha wakulima kukusanya mazao yao kwa kuzingatia ubora na kuuza kwa pamoja kwa lengo la kupata bei nzuri kulingana na mwenendo wa soko. Mazao yatakayohifadhiwa katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yatauzwa haraka iwezekavyo ndani ya **siku 30** tangu tarehe ya kuandikwa na kutolewa kwa Stakabadhi ya ghala husika na bei kuridhiwa na wakulima husika.

**SEHEMU YA TATU**
**USIMAMIZI WA GHALA KUU**

Ili kufanikisha ukusanyaji na uuzaji mazao ya *choroko, mbaazi, dengu, ufuta na soya.* Utaratibu ufuatao utatumika katika Ghala Kuu zilizopewa leseni chini ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala.

**Wajibu wa Mwendesha Ghala k [illegible] Mazao**

i. Kupokea mazao yanayokidhi viwango vya ubora vya Shirika la Viwango Tanzania kama ifuatavyo: -.
   a. Daraja la Kwanza **(GRADE 1)**, Daraja la Pili **(GRADE 2)** na Daraja la Tatu **(GRADE 3)** kwa mujibu wa Viwango kama ifuatavyo: -

| Na. | Aina ya Zao | Kiwango Namba |
|---|---|---|
| 1 | Choroko | TZS 1666:2014 |
| 2 | Dengu | EAS: 754:2013 |
| 3 | Soya | TZS 1083:2018/EAS 762:2017 |
| 4 | Mbaazi | TZS 1084:2014-EAS 756:2013 |
| 5 | Ufuta | TZS 741: 2018 |

ii. **Mazao Bila Daraja (BD)** yatapokelewa ghalani kwa makubaliano kati ya Mwendesha Ghala na Mweka Mali baada ya vigezo vifuatavyo kuhakikiwa: -

a. Rangi ya Jamii ya kunde;
b. Kiwango cha unyevu;
c. Kiwango cha uchafu *(foreign matter);*
d. Kiwango cha mbegu zilizooza;
e. Kiwango cha mchanganyiko wa mbegu nyingine.
f. Umbo

Viwango vitakavyotumika katika sehemu a, b, c, d na e hapo juu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali hapo chini.

| Na | Aina ya Zao | (b) | (a), (c), (d) na (e) |
|---|---|---|---|
| 1 | Choroko | ISO 24557:2009 | ISO 605:1991 |
| 2 | Dengu | ISO 24557:2009 | ISO 605:1991 |
| 3 | Soya | ISO 24557:2009 | ISO 605:1991 |
| 4 | Mbaazi | ISO 24557:2009 | ISO 605:1991 |
| 5 | Ufuta | ISO 665:2000 | ISO 658:2002 |

iii. Cheti cha Ubora wa zao la Jamii ya Kunde kitakachotumika ni *Fomu Namba 3* inayopatikana katika tovuti ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala;

iv. Kuwa na vifaa muhimu vya kupima vigezo vya ubora ambavyo vitajumuisha,

a. Chekeche ya maabara *(Laboratory Analysis Sieve),*
b. Kipima unyevu *(Moisture Meter)* cha zao la jamii ya kunde;
c. Mizani ya maabara iliyothibitishwa na Wakala wa Vipimo;
d. Bambo ya kuchukulia sampuli kutoka kwenye vifungashio;
e. Vijiko vya maabara vinavyotosheleza mahitaji ya upimaji wa sampuli
f. Bakuli za kupimia sampuli;
g. Mashine ya kushona vifungashio.

v. Kuhakikisha kuwa vifungashio vyote vina jina kamili la Mweka Mali;

vi. Kuhakikisha kila kifungashio kitakachotumika katika kujaza mazao yaliyomwagika ghalani ni kipya na kina alama ya utambulisho ya Mwendesha Ghala.

vii. Kupokea na kuhakiki Hati ya Ankara ya Mauzo (Invoice), Toleo la Kutoa Mazao Ghalani (Release Warrant), na Stakabadhi ya Ghala husika kabla ya kutoa jamii ya kunde ghalani;

viii. Kuhakiki idadi ya vifungashio vya jamii ya kunde vinavyotolewa ghalani kulingana na Stakabadhi husika;

ix. Kutoa kwa Mnunuzi Hati ya Toleo la Stakabadhi *{Warehouse Receipt Issue Note (WRIN)}* kwa kila Jamii ya kunde inayotolewa ghalani;

x. Kutoa taarifa ya mapokezi *(Fomu Namba 5)* na ya utoaji *(Fomu Namba 6)* kila siku kwa Jamii ya Kunde itakayopokelewa au kutolewa ghalani kwenye kanzidata ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala;

xi. Kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) malipo ya madai ya aina yoyote yaliyothibitishwa na Bodi kwenye Akaunti ya Kinga ya Utendaji ya Bodi.

**Viwango vya Utendaji katika Ghala Kuu Kwenye Mfumo wa Stakabadhi Za Ghala Mazao Jamii ya Kunde**

i. Vifungashio vyote vitakavyotumika katika zao la Jamii ya Kunde vitakuwa vipya na vinavyokidhi kiwango cha kimataifa **ISO 23560:2015** na kuidhinishwa na Shirika la Viwango Tanzania ambapo; uzito wa kila kifungashio ni **gram 100,** urefu wa nje **milimita 965** na upana wa nje **milimita 560;**

ii. Uzito wa jamii ya kunde katika kila kifungashio ghalani ni **kilogram 50.** Iwapo vifungashio vitakuwa havina uzito wa **kilogram 50** za Jamii ya kunde, ni wajibu wa Mweka Mali kufananisha vifungashio vyote kwa lengo la kupata uzito wa **kilogram 50** kwa kila kifungashio;

iii. Kiwango cha juu cha urefu wa steki ya vifungashio vya jamii ya kunde usizidi mita tatu kutoka kwenye chaga;

iv. Viwango vya Unyevu wa mazao Jamii ya Kunde zitakazopokelewa ghalani utakuwa kama ifuatavyo.

| Na | Aina ya Zao | Kiwango Kisizidi |
|---|---|---|
| 1 | Choroko | 11.50% (w/w) |
| 2 | Dengu | 8.50% (w/w) |
| 3 | Soya | 8.50% (w/w) |
| 4 | Mbaazi | 8.50% (w/w) |
| 5 | Ufuta | 7.50% (w/w) |

i. Sampuli ya Jamii ya kunde kwa ajili ya kuhakiki ubora itachukuliwa kwa kufuata utaratibu wa kiwango namba **TZS 873:2006/ISO 24333;**

ii. Nyaraka za ndani ambazo ni lazima zitumike katika ghala lililosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ni:-

**Wakati wa Kupokea mazao Jamii ya Kunde Ghalani: -**

a) Hati ya Mweka Mali ya kukabidhi mazao Jamii ya Kunde ghalani – *"Produce Delivery Note"* (PDN);
b) Hati ya kuhesabu idadi ya vifungashio – *"Tally Sheet" (TS);*
c) Hati ya kupima uzito – "*Weight Note" (WN);*
d) Cheti cha Ubora – *"Quality Certificate" (QC);*
e) Hati ya kupokea jamii ya kunde ghalani – *"Goods Received Note" (GRN)*.

**Wakati wa Kutoa jamii ya kunde ghalani: -**

a. Nakala ya Ankara ya mauzo ya Jamii ya kunde – *"Sales Invoice"*;
b. Hati ya Toleo la Jamii ya kunde kutoka benki au kwa muuzaji – *"Release Order (Warrant)";*
c. Agizo la kuchukua jamii ya kunde ghalani kutoka kwa Mnunuzi – *"Dispatch Order";*
d. Hati ya kuhesabu idadi ya vifungashio – *"Tally Sheet" (TS);*
e. Hati ya kupima uzito – *"Weight Note" (WN);*
f. Hati ya kutoa Jamii ya kunde Ghalani – *"Warehouse Receipt Issue Note" (WRIN)*

**Nyaraka Nyingine***;*

a. Rejesta katika Idara mbali mbali;
b. Bin Card katika kila steki iliyopo katika ghala la kuhifadhi jamii ya kunde;

i Kitabu cha Ukaguzi wa Taarifa za Ghala za Kila Siku;

ii. Upungufu wa idadi ya vifungashio vya jamii ya kunde katika Stakabadhi yoyote hauruhusiwi na iwapo ikitokea Mwendesha Ghala atalipa kwa thamani ya bei ya soko pamoja na adhabu ya asilimia 20%;

iii. Stakabadhi yoyote itakayobakia bila kuwa na mazao ghalani ni ukiukwaji wa viwango vya utendaji wa Mwendesha Ghala husika. Stakabadhi hii italipwa kwa bei ya soko pamoja na adhabu ya asilimia 20%. Mwendesha Ghala atatoa taarifa ya upotevu wa mazao ghalani katika kituo cha Polisi cha karibu ndani ya saa 24 tangu kubainika kwa tukio na kuwasilisha taarifa hiyo Bodi;

iv. Muda wa kuhifadhi Jamii ya Kunde bila malipo ya ziada kwa mnunuzi ni siku saba (7) za kazi tangu tarehe ya mauzo;
v. Baada ya siku saba (7) za kazi tangu tarehe ya mauzo kumalizika, Mnunuzi atalazimika kulipia gharama ya ziada ya kuhifadhi mazao ya Shilingi 3.0/= kwa kilo kwa siku, kwa siku 30 zinazofuata;
vi. Mwendesha Ghala anaruhusiwa kutoa ilani ya Agizo la Kutoa mazao ghalani kwa mnunuzi mara tu inapotimia siku ya 37 tangu tarehe ya mauzo. Ilani hii itadumu kwa muda wa siku 7 tangu tarehe ya kuandikwa kwake;
vii. Mnunuzi atahesabiwa ameshindwa kabisa kutoa Jamii ya kunde ghalani baada ya siku 44 tangu siku ya mauzo;
viii. Gharama za Mwendesha Ghala kuhifadhi Mazao ghalani (Handling Charges) isiyozidi Shilingi 38 kwa kilo. Gharama hii itaandikwa kwenye Stakabadhi na italipwa na Mnunuzi mara moja kwa kila kilo iliyoandikwa kwenye Stakabadhi.
ix. Gharama zote zimejumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (V.A.T) na kodi nyingine za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
x. Muda wa kuhifadhi jamii ya kunde kwa Mweka Mali (Muuzaji) ni siku 93 tangu tarehe ya kuandikwa Stakabadhi husika. Iwapo kutakuwepo na tatizo la soko, Mweka Mali au Wakala wake atatakiwa kuomba Bodi ruhusa ya kuongezewa muda wa ziada. Uamuzi wa kuongezewa muda na gharama zake utatolewa na Bodi;
xi. Mazao Jamii ya Kunde yatakayoshindikana kutolewa ghalani katika kipindi kilichotajwa katika kipengele cha (xv) itauzwa kwa utaratibu uliowekwa na Bodi kwa lengo la kulipa stahiki mbali mbali kwa wahusika kwa mujibu wa sheria;
xii. Jamii ya kunde ambazo zitafikishwa ghalani zikiwa na uchafu, unyevu mkubwa, idadi ya vifungashio isiyolandana na uzito na utofauti wa kumbukumbu hazitapokelewa na Mwendesha Ghala.
xiii. Katika hali ya utata wa aina yoyote, idhini ya mwisho ya kutoa mazao mazao ghalani itatolewa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.
xiv. Mnunuzi ahakikishe ubora wa mazao kabla ya kuyatoa ghalani

## UKUSANYAJI WA CHOROKO, UFUTA, SOYA, MBAAZI NA DENGU KWENDA GHALA LA MNADA

3.1 Kila mkulima mwenye Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kwa ajili ya kuuza atapeleka katika ghala la Chama cha Msingi akiwa amezipanga kwenye madaraja yanayotambulika kwa mujibu wa Miongozo huu.

3.2 Chama cha Ushirika cha Msingi kitahakikisha kuwa kabla ya msimu wa ununuzi kuanza, mzani unaotumika kupimia Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu katika ghala lake unakaguliwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) chini ya sheria ya vipimo na mizani hapa nchini.

3.3 Chama cha Ushirika cha Msingi kitapokea Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengukutoka kwa wakulima, kuzipima kwa mzani uliokaguliwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania na kuziweka katika magunia mapya yenye viwango vya ubora vilivyothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

3.4 Chama cha Ushirika cha Msingi kitahakikisha kuwa uzito halisi wa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu ni **kilo 50** kwa kila gunia kabla ya kupeleka kwenye ghala la mnada.

3.5 Chama cha Ushirika cha Msingi kitaandika jina la chama chake na namba ya utambulisho iliyotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kila gunia la Dengu, Choroko, Ufuta, Mbaazi na Soya.

3.6 Chama cha Ushirika cha Msingi kitapeleka Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu za wakulima wake kwenye ghala la mnada lililosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na lililo karibu yake kwa ajili ya mauzo.

3.7 Chama cha Msingi kitasafirisha Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu za

wakulima kwenda ghala la mnada kwa kutumia PDN ya Chama cha Ushirika cha Msingi ikiambatana na fomu ya orodha ya wakulima iliyojazwa kikamilifu ya wamiliki wa Dengu husika ikiwa katika nakala nne; nakala ya kwanza ipelekwe kwa Afisa Ushirika Msimamizi wa ghala husika, nakala ya pili Chama Kikuu husika, nakala ya tatu ipelekwe kwa Mtunza Ghala la mnada na nakala ya nne ibaki katika Chama cha Msingi chenyewe.

3.8 Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupitia Maafisa Ushirika wake na wa Halmashauri husika watakokotoa gharama ya kusafirisha Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu husika kwa kuzingatia umbali halisi kati ya Chama cha Ushirika cha Msingi husika na ghala la mnada.

3.9 Mtunza Ghala atatakiwa kupokea Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu zilizo katika ubora wa daraja la kwanza, daraja la pili na daraja la tatu na kuzipanga katika “loti” tofauti kwa kuzingatia madaraja kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa zao husika wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inayotolewa kila mwaka.

3.10 Mtunza Ghala anatakiwa kutunza na kuzitoa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kwa mnunuzi husika zikiwa katika ubora na kiasi kama alivyozipokea kutoka Chama cha Ushirika cha Msingi.

**SEHEMU YA NNE**

**UHAKIKI WA UBORA WA CHOROKO, UFUTA, SOYA, MBAAZI NA DENGU GHAFI**

4.1 Mtunza Ghala atatakiwa kuajiri mhakiki wa ubora wa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu aliyefuzu mafunzo na kupata cheti kutoka Chuo cha Kilimo kinachotambulika na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama inavyoelekezwa kwenye taratibu za wafanyakazi wa mwendesha Ghala na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

4.2 Mtunza Ghala atatakiwa kuwa na vifaa vya uhakiki wa ubora wa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu vilivyopitishwa na kutambulika na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

4.3 Mnunuzi akishakabidhiwa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu alizonunua mnadani atawajibika kulinda na kuhifadhi ubora hadi anaposafirisha.

4.4 Mnunuzi aliyeshinda mnada na kulipia Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu husika endapo atahitaji kujiridhisha ubora wa mzigo aliolipia kabla ya kuziondosha kutoka ghala la mnada, atatakiwa kutoa taarifa kwa maandishi kwa Meneja wa Mtunza Ghala husika. Mhakiki wa Ubora wa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kwa Mtunza Ghala ndiye atakayehakiki ubora wa mzigo mbele ya mnunuzi husika.

4.5 Endapo kutatokea mgogoro wa ubora wa Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu taratibu za kisheria zilizowekwa zitafuatwa.

**SEHEMU YA TANO**
**UNUNUZI WA CHOROKO, UFUTA, SOYA, MBAAZI NA DENGUGHAFI**

5.1 Wanunuzi wanaonunua Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu ghafi kupitia soko la Bidhaa Tanzania, watajisajili Soko la bidhaa na kuweza kushiriki kununua mazao hayo popote nchini kwa njia ya kielektroniki.

5.2 Biashara ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu itatumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuuzwa kupitia Soko la Bidhaa.

5.3 Mnunuzi atatakiwa kuzingatia Sheria ya Stakabadhi za ghala sura 339 (RE) 2016 kanuni na Taratibu za soko la bidhaa 2016 na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika katika msimu husika.

5.4 Mnunuzi atatakiwa kuzingatia masharti na vigezo vya mnada wa mauzo ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kama yalivyotolewa katika mwongozo huu.

**SEHEMU YA SITA**
**MALIPO MBALIMBALI**

6.1 Wakulima watalipwa fedha zote za malipo ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kwa mkupuo mmoja kupitia akaunti zao za benki kulingana na bei halisi ya mazao hayo kwenye mnada husika baada ya kutoa tozo zilizopo kisheria na zilizokubalika na wadau.

6.2 Malipo yatafanyika kupitia akaunti ya benki iliyosajiliwa kwa jina lake au namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina lake siku mbili za kazi baada ya siku ya mnada (masaa 48) na endapo mnunuzi amechelewa basi ataongezewa siku moja (Siku ya kazi) ikiwa na adhabu ya asilimia tano (5) ya fedha aliyotakiwa kulipa (kiasi hicho kitaumika kufidia wakulima husika) .

6.3 Soko la bidhaa litahamisha kiasi hicho cha fedha kwenda Chama Kikuu husika ndani ya saa 24 siku za kazi kupitia Akaunti ya pamoja (collectiom AC). Chama Kikuu kitafanya malipo kwa wakulima na wadau wengine ndani ya siku 5 baada ya mnada

**N.B** Chama kikuu kinatakiwa kufungua ***akaunti ya pamoja*** (collection A/C) kwa ajili ya kupokea pesa kutoka soko la Bidhaa ili kufanya malipo kwa wakulima

6.4 Gharama za uendeshaji ghala ya mnada zitalipwa na mnunuzi kwa kilo kabla kuondosha mzigo.

6.5 Maafisa Ushirika wa Wilaya, viongozi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu kwa kuwashirikisha wakulima watakokotoa na kuridhia gharama halisi za usafirishaji wa Dengu, Choroko, soya, mbaazi na Ufuta kwenda Ghala la mnada kwa kuzingatia umbali halisi.

## SEHEMU YA SABA
## UENDESHAJI WA MINADA YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, MBAAZI NA SOYA

### 7.1 UTARATIBU WA MAUZO KATIKA ZAO LA CHOROKO, DENGU, UFUTA, MBAAZI NA SOYA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 70A (1) cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala, mauzo ya bidhaa katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yatafanyika kupitia Soko la Bidhaa (Commodity Exchange) linaloendeshwa na Tanzania Merchantile Exchange (TMX).

Mnunuzi anatakiwa kulipa kinga ya dhamana kutokana na viwango vitakavyooneshwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

7.2 Kamati ya Biashara ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu katika msimu husika itaundwa na wajumbe wafuatao: -

a) Katibu Tawala wa Mkoa
b) Mwakilishi wa Ofisi ya Mrajis;
c) Chama Kikuu cha Ushirika (Mwenyekiti na Meneja Mkuu);
d) Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri (Mtaalaam wa Kilimo);
e) Mwakilishi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala;
f) Mwakilishi wa Soko la Bidhaa Tanzania
g) Mwakilishi Chama cha Msingi (Mwenyekiti/Katibu)
h) Wawakilishi wa wakulima
i) Taasisi za kifedha

7.3 Uamuzi wa kuuza Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kupitia mnada husika kwa munuzi ni wakulima.

7.4 Chama cha Ushirika cha Msingi kitawasilisha stakabadhi (*Wareheouse Receipt*), fomu iliyojazwa orodha ya wakulima na hati ya ubora wa zao zilizopokelewa katika ghala la mnada kwa Chama Kikuu husika.

7.5 kwa mujibu wa 70a (1) cha sheria ya stakabadhi za ghala, mauzo ya bidha akatika mfumo wa stakabadhi za ghala yatafanyika kupitia Soko la Bidhaa (TMX), kila mnunuzi ataweka kinga ya zabuni kwa fedha taslimu (*Bid Security*) kwenye akaunti ya malipo ya soko la Bidhaa Kabla ya kushiriki mnada. Kiasi hicho kitatumika kufidia wakulima endapo mnunuzi atashindwa kulipa mazao aliyoshinda mnadani au kitarejeshwa ndani ya saa 24 siku za kazi toka mnunuzi atakapotoa taarifa Soko la Bidhaa juu ya urejeshwaji wake. Kiasi hicho kinaweza kutumika kama malipo ya awali kwa mnunuzi anayelipia mzigo wa mwisho.

7.6 Soko la Bidhaa liandae Sales Catalogue kwa kushirikiana na chama kikuu kulingana na jinsi choroko, ufuta, soya, mbaazi na dengu zilivyoingia ghalani na mzigo wote ulioko ghalani kuuzwa kadri ya sales catalogue.

7.7 Ofisi ya Mrajis kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika wataandaa ratiba itakayoonesha siku na mahali pa kufanyia minada na kuwatangazia wadau.

7.8 Soko la bidhaa litatoa Hati ya Madai (Sales Invoice) na kumpa mnunuzi ndani ya saa 12 baada ya wakulima kuridhia kuuza mazao yao. Viongozi na watendaji wa Vyama Vikuu vya Ushirika watashuhudia minada ili kurahisisha zoezi la wakulima kuridhia bei zitakazokuwa zimepatikana na kuitaarifu Soko la Bidhaa kwa wakati kwa kupitia fomu maalum ya kuridhia..

7.10 Mnunuzi aliyeshinda atafanya malipo ndani ya siku 2 za kazi baada yamnada.

7.11 Mnunuzi hatapewa agizo la toleo la mzigo (Release Order/Warranty) na Soko la Bidhaa mpaka akamilishe malipo yote kwa ankara ya mauzo husika.

7.12 Mnunuzi hatoruhusiwa kushiriki mnada unaofuata iwapo atakuwa hajakamilisha malipo ya mnada uliopita kwa muda uliowekwa.

7.13 Mauzo yoyote ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu yatakayofanywa nje ya utaratibu na nje ya Mwongozo huu yatakuwa batili na mzigo huo utataifishwa na kuwa mali ya halmashauri husika na waliohusika watachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria.

7.14 Kabla ya mauzo, Chama Kikuu cha Ushirika kitatoa taarifa ya malipo ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu zilizonunuliwa katika mnada uliotangulia na Meneja atasaini nyaraka ya taarifa hiyo.

**SEHEMU YA NANE**

**UTOAJI WA TAARIFA ZA MAUZO YA DENGU, CHOROKO, UFUTA, MBAAZI NA SOYA**

8.1 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania watatoa taarifa za mwenendo wa soko la Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kila wiki kipindi cha msimu wa ununuzi kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio za kijamii zilizopo katika Halmashauri zinazozalisha mazao hayo na tovuti za taasisi hizo.

8.2 Mrajisi Msaidizi wa Mkoa atawajibika kutoa taarifa kwa AMCOS na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kuhusu mauzo ya Dengu, Choroko, Ufuta, Mbaazi na Soya.

8.3 Kila Chama cha Msingi kitabandika taarifa za mauzo ya Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu za wakulima wake kwenye mbao za matangazo za chama chake.

## SEHEMU YA TISA

## USAFIRISHAJI WA DENGU, CHOROKO, UFUTA, MBAAZI NA SOYA

9.1 Mnunuzi atasafirisha Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

9.2 Mnunuzi atasafirisha Choroko, Ufuta, Soya, Mbaazi na Dengu kwa kutumia PDN inayotolewa na Chama husika pamoja na nyaraka zote halali za ununuzi wa mazao.

9.3 Uongozi wa Halmashauri kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama utahakikisha kuwa mazao yote yanayosafirishwa ni yale yaliyonunuliwa kwenye mnada

**SEHEMU YA KUMI**
**USULUHISHI WA MIGOGORO**

10.1 Mgogoro wa aina yeyote baina ya upande mmoja na mwingine utatatuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.06 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015, na Sheria Stakabadhi za Ghala sura 339RE 2016 Pamoja na Sheria ya Soko la Bidhaa ya mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2016.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## TOZO MBALIMBALI

Mwongozo unaainisha tozo mbalimbali ambazo zitalipwa na mnunuzi. Tozo hizo ni kama zifuatazo: -

| **Aina ya tozo** | **Kiasi Tsh kwa kilo** |
|---|---|
| Chama kikuu cha Ushirika | 20 |
| Chama cha Ushirika cha msingi | 50 |
| Vifungashio | 20 |
| Cess | 3% ya *Farm Gate Price* |
| Usafiri kutoka kwenye Amcos kwenda ghala la mnada | Gharama zitakokotolewa kulingana na umbali |
| Gharama za Mtunza Ghala | Tsh 38 |
| Tmx | Tsh 1 |

***N.B. Gharama hizi zinalipwa na mnunuzi***

***Mwongozo huu umetolewa leo tarehe***……19/01/2021…………………………… ***na***

……………………………
***Dkt. Benson O. Ndiege***
***MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA***

Warehouse Receipts Regulatory Board
P. O. Box 38093
Dar es Salaam

……………………………
***Asangye N. Bangu***
***KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA***

TANZANIA MERCANTILE EXCHANGE PUBLIC LIMITED COMPANY
P.O.Box 31032
DAR-ES-SALAAM

……………………………
***Godfrey Malekano***
***AFISA MTENDAJI MKUU SOKO LA BIDHAA TANZANIA***